

- Taarifa wanazopatiwa wahudumu wa afya ziwe za kisayansi na za kweli;
- Taarifa na maelezo kuhusu ulishaji mbadala ikijumuisha zilizoko kwenye lebo, lazima zieleze faida za kunyonyesha pamoja na gharama na matatizo yanayoambatana na ulishaji mbadala;
- Maziwa ambayo hayafai kulisha watoto wachanga kama vile maziwa yaliyoongezwa sukari kiwandani yasitangazwe kuwa yanaweza kutumika kulisha watoto wachanga;

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania
S.L.P. 977, Dar es Salaam
Simu: 255-22-2118137-9
Fax: 255-22-2116713
E-mail: tfnc@muchs.ac.tz

Kimetayarishwa na:
Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania
kwa uhisani wa UNICEF



IJUE SHERIA INAYODHIBITI UUZAJI NA USAMBAZAJI WA MAZIWA NA VYAKULA VYA WATOTO



Kijarida kwa Wafanyakazi wa Afya

Utangulizi:

Sheria ndogo ya kudhibiti uuzaji na usambazaji wa maziwa na vyakula vya watoto wadogo Tanzania imetokana na kanuni ya kimataifa inayodhibiti uuzaji na usambazaji wa maziwa na vyakula vya watoto wadogo. Sheria hii ndogo ipo chini ya sheria ya Chakula (Udhibiti wa ubora wa vyakula Na. 10 ya 1978), na ilianza kutumika rasmi mwaka 1994.

Nini Madhumuni ya sheria hii?

Sheria hii ndogo inalenga katika kulinda, kuhimiza na kuendeleza unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa kudhibiti uuzaji na usambazaji holela wa maziwa na vyakula vya watoto.

Kwa nini sheria ilitungwa?

Iligundulika kuwa matangazo ya kibiashara ya maziwa na vyakula vya watoto yanaathiri unyonyeshaji. Sheria hii imeundwa ili kudhibiti matangazo hayo.

Upeo wa sheria hii ndogo ni upi?

Sheria hii ndogo inahusu maziwa, vyakula na vinywaji vyote vinavyouzwa kama mbadala wa maziwa ya mama. Hivi ni pamoja na maziwa ya kopo ya watoto, maziwa mengine, vyakula vya watoto na juisi.

Pia, chupa za kulishia watoto pamoja na nyonyo bandia navyo vinahusika. Sheria haizuii uuzaji wa vyakula hivi isipokuwa jinsi vinavyotangazwa.

Nani anahusika katika utekelezaji wa sheria hii?

- Watengenezaji na wasambazaji wa vyakula vya watoto wanawajibika kukubaliana na matakwa ya sheria.

- Watoa huduma za afya, wanapaswa kuelewa barabara sheria hii na mipaka yake ili kutimiza wajibu wao wa kulinda lishe na afya ya mama na mtoto kutokana na utangazaji wa kibiashara.

Utajuaje kama matangazo ya kibiashara yanapingana na malengo ya sheria?

Kama tangazo halitoi umuhimu unaostahili au linapunguza thamani ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama, litakuwa linapingana na malengo ya sheria.

Sheria hii haikatazi:

- Uzalishaji na upatikanaji wa maziwa mbadala na vyakula vingine vya watoto wachanga.
- **Matumizi sahihi** ya vyakula vya nyongeza baada ya mtoto kutimiza umri wa miezi 6 au matumizi ya vyakula hivyo kwa mtoto aliye chini ya umri wa miezi 6 endapo itashauriwa na daktari.

Ni njia zipi ambazo makampuni yanayotengeneza maziwa na vyakula vya watoto yanaingilia mfumo wa huduma za afya na hivyo kuathiri unyonyeshaji.

Kwa kutoa:

- Sampuli za bure za maziwa na vyakula hivyo kwa wanawake;
- Mabango yanayoonyesha majina au nembo za kampuni;
- Maandiko na zawadi zenye majina ya

kampuni kwa watoa huduma wa afya na wanawake-,

- Vijarida vya kampuni vinavyohusu unyonyeshaji au matunzo ya watoto;
- Maandiko yanayotangaza bidhaa kwa watumishi wa afya;
- Ufadhili wa matukio ya kitaalamu au washiriki wanaohudhuria, mfano semina.

Vipengele muhimu katika sheria hii:

Sheria hii inajumuisha vipengele 9 muhimu:

- Hairuhusu kufanya matangazo ya biashara ya uuzaji wa maziwa ya kopo na vyakula vingine vya watoto kwa umma;
- Hairuhusu kutoa sampuli za bure za maziwa hayo kwa wanawake au familia zao;
- Hairuhusu uwekaji matangazo kwenye vituo vinavyotoa huduma za afya;
- Hairuhusu wafanyakazi wa kampuni zinazouza maziwa ya kopo kuwashauri wanawake kuhusu ulishaji wa watoto;
- Hairuhusu utoaji wa zawadi au sampuli kwa wahudumu wa afya;
- Hairuhusu kuweka picha za watoto wachanga kwenye lebo zinazosifia ulishaji wa maziwa au vyakula vya watoto;